



City of Grand Rapids
Office of Oversight and Public Accountability
300 Monroe Ave. NW Suite 499
Grand Rapids, MI 49503
o: (616) 456-4OPA e: opa@grcity.us
Brandon D. Davis, Esq. - Director

Uwasilishaji wa Lalamiko

Mtu yeote yule anaweza kuwasilisha lalamiko dhidi ya mfanyakazi wa Idara ya Polisi ya Grand Rapids kwa kupiga simu, kutembelea, ama kutuma barua pepe kwenda Ofisi ya Usimamizi na Uwajibikaji wa Umma (OPA).

Lalamiko hutathminiwa namna gani?

Lalamiko likishapokelewa, ofisi ya OPA hulipitia, kisha hulituma kwenda Kitengo cha Mambo ya Ndani cha GRPD (IAU) kwa ajili ya kushughulikwia. Kila lalamiko hutathminiwa ili kuona kama lalamiko hilo:

- linakiuka sera ya GRPD
- lina taarifa za kutosha kutambua uzito wa lalamiko, ama
- ni zaidi ya tukio dogo au lililotengwa na si jambo ambalo teyari limekwisha kutatuliwa ama kushughulikiwa.

Ofisi ya Mambo ya Ndani Inapitia Mchakato na Sera ya Lalamiko Hilo

Ofisi ya mambo ya ndani inashughulikia lalamiko hilo na inaelekeza mwelekeo, kulingana na kweli na hali zilizopo, na Sera na Michakato ya GRPD. Mielekeo ya lalamiko imegawanywa kama ifuatavyo:

Lisilo na Msingi: Uchunguzi umethibitisha kwamba jambo linalolalamikiwa halikutokea. (Hii huhesabika pia pale jambo husika linapokuwa limepotokea, lakini wafanyakazi walijotajwa hawakuhusika.)

Limeondolewa: Kitendo husika, kilichoweka msingi wa lalamiko hilo ama lawama hiyo, kilitokea; hata hivyo, uchunguzi umebainisha kwamba kutokea kwa kitendo hicho kulifuata haki, sheria na kilikuwa sahihi.

Halijakubalika: Uchunguzi umeshindwa kubainisha ushahidi wa kutosha kuthibitisha shutma zilizolezwa kwenye lalamiko ama kuweza kufikia thibitisho la kukanusha shutma hizo.

Limekubalika: Uchunguzi umebainisha ushahidi wa kutosha kuthibitisha shutma iliyolezwa kwenye lalamiko. Ukiukwaji wa sera na/ama mchakato ulitokea, na hatua stahiki za kiutawala zitachukuliwa.

Lalamiko linaweza pia kuainishwa kama Lililofungwa na Utawala, jambo linalomaanisha kwamba lalamiko hilo limerekodiwa lakini halijachunguzwa, au kuondolewa – mlalamikaji kuondoa lalamiko husika.

Iwapo kama mwelekeo utaafiki kuwa lalamiko halijakubalika, halina msingi, au kwamba afisa husika ameondolewa mashtaka, mlalamikaji anaweza kukata rufaa kwa CAB kupata mapitio zaidi ya kesi hiyo.

Je, uwasilishaji wa lalamiko ni salama?

Tunaudhamiria mchakato wetu kuwa salama. Hautaulizwa maswali kuhusiana na hadhi yako ya uhamiaji. Hautahitajika kuzungumza na mfanyakazi wa GRPD uliyeweka lalamiko dhidi yake.

OPA hufanya kazi kusaidia wanajamii kuitia mchakato wake, katika namna inayosaidia kuhakikisha kwamba watu wote wanajihisi salama na wanakuwa salama katika nyakati zote ndani ya jamii yetu.

Ninawasilishaje lalamiko?



**WASILISHA LALAMIKO KWA OFISI YA USIMAMIZI & UWAJIBIKAJI WA UMMA KUPITIA
BARUA PEPE:**

opa@grcity.us



PIGA SIMU KWENDA OFISI YA USIMAMIZI & UWAJIBIKAJI WA UMMA:

(616) 456-4OPA

Kama simu yako itapelekwa katika mfumo wa ujumbe wa sauti, tafadhali acha ujumbe na mmoja wa wafanyakazi atakurudia hivi punde. Tafadhali hakikisha kwamba unaacha taarifa zako za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na anuani ya barua pepe ndani ya ujumbe huo.



TEMBELEA OFISI YA USIMAMIZI & UWAJIBIKAJI WA UMMA:

**Barabara ya 300 Monroe, NW, Jengo 499
Grand Rapids, MI 49503**

Masaa yetu ya kazi ni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, **8:00 asubuhi - 5:00 jioni**.



TUANDIKIE BARUA:

**Ofisi ya Usimamizi na Uwajibikaji wa Umma
Barabara ya 300 Monroe, NW, Jengo 499
Grand Rapids, MI 49503**

OPA inafurahia kutoa huduma za ana kwa ana za utafsiri wa lugha ya Kihispania. Tafadhali tujulishie kama utahitaji Mkalimani.



www.grcity.us/opa

<http://www.grandrapidsmi.gov/opa>